JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MAFUNZO YA VIONGOZI KATIKA NGAZI YA KIJIJI, MTAA NA KITONGOJI

MIPANGO SHIRIKISHI YA MAENDELEO KATIKA NGAZI YA MTAA, KITONGOJI NA KIJIJI

8

DODOMA
APRILI, 2001

YALIYOMO

Uk.

1. Yaliyomo ii

2. Utangulizi..... 1

3. Sifa za Kiongozi Mwezeshaji..... 1

4. Mpango Shirikishi wa Maendeleo ya Kijiji/Mtaa..... 1

5. Mwisho..... 5

MIPANGO SHIRIKISHI YA MAENDELEO KATIKA NGAZI YA MTAA, KITONGOJI NA KIJIJI

1. UTANGULIZI

Maendeleo ni kupiga hatua ya kudumu ya maisha kutoka hali ya sasa kwenda katika hali bora zaidi iliyowekewa malengo katika mpango.

Mpango ni utaratibu wa jamii kuweka malengo ya maendeleo na utekelezaji wake katika kutatua matatizo yao kwa kutumia rasilimali mbalimbali ili kuboresha hali ya maisha yao kwa kuzingatia mazingira halisi.

2. Sifa za Kiongozi Mwezeshaji:

Katika kufanikisha maandalizi ya mipango shirikishi kiongozi katika ngazi ya Kijiji, Kitongoji na Mtaa anatarajiwa kuwa na sifa zifuatazo:-

- Awe na upeo na mwelekeo wa kubadili hali za maisha kutoka hatua moja hadi nyingine, kwa kutilia maanani ilipo jamii na inakotaka kwenda.
- Awe na stadi na mbinu za uongozi kumwezesha kuandaa mikutano iliyoelekezwa kisheria pamoja na kuweka kumbukumbu za mikutano pamoja na orodha (rejista) ya wakazi wote.
- Awe mwajibikaji, anayejua majukumu yake kisheria, kiutaratibu na dhamana yake kwa watu waliomweka.
- Awe muwazi, mkweli na mwaminifu katika kutoa habari kwa washirika/washikadau zinazohusiana na fursa, vikwazo, vyanzo vya mapato, ukusanyaji na matumizi ya mapato ili kuwezesha kuandaa mipango na bajeti halisi.
- Awe na ufahamu wa masuala ya jinsia ili kuwezesha

kuwepo kwa majadiliano kati na baina ya makundi mbalimbali yaliyopo katika jamii; kwa mfano wazee, wanawake, vijana, walemavu, pamoja na makundi ya kiuchumi-jamii (wafugaji, wakulima n.k.).

- Awe na mbinu na stadi za mawasiliano kuiwezesha jamii kupeana na kubadilishana uzoefu na habari za kuongeza uwezo wake kimaarifa na kiufundi ili kupata ufanisi katika shughuli zake.
- Ili kuwa muwazi, mkweli na mwaminifu kiongozi asijishirikishe katika wizi, udanganyifu, rushwa, ubaguzi, ubinafsi, au kuongoza kwa kurubuni.

Kwa kuzingatia sifa hizi kiongozi anatarajiwa awezeshe uandaaji na utekelezaji wa Mpango Shirikishi wa Maendeleo katika eneo lake.

3. Mpango Shirikishi wa Maendeleo ya Kijiji/Mtaa

- **Mpango Shirikishi** ni mfumo wa upangaji unaozingatia majadiliano, katika kuchambua matatizo na fursa za utatuzi; kwa kuhusisha walengwa wote, kijinsia, kiumri, kiuchumi-jamii, ili hatimaye kufikia maafikiano ambayo yanawekewa kumbukumbu kama mpango.
- **Mpango** lazima uwe na Bajeti ambayo ni makadirio ya gharama zinazowezesha kufanyika kwa shughuli zilizopangwa ili kufikia malengo.
- **Upangaji Mpango Shirikishi**

  Wajibu mkuu wa kiongozi katika upangaji mpango shirikishi ni kuwezesha walengwa katika hatua mbalimbali wakutane, wajadiliane na hatimaye kuafikiana kuhusu mpango wao na utekelezaji wake kwa kuzingatia maoni na ushauri wa kitaalam.
- Upangaji Mpango Shirikishi huenda hatua kwa hatua kama ifuatavyo:

a) **Kuunda Timu ya Wawezeshaji Shirikishi**

- Mkutano wa viongozi (Halmashauri ya Kijiji/Mtaa).
- Katika mkutano huu Timu ya Wawezeshaji Shirikishi huundwa ikijumuisha Wataalamu (Ugani) na baadhi ya Viongozi na wanajamii/wanakijiji.
- Kwa kawaida, Timu hii hugawanywa katika makundi madogo yatakayofanya kazi katika sehemu mbalimbali za kijiji, (vitongoji) mtaa. Kila kundi dogo la Timu ya wataalam shirikishi liwe na walau na Wataalam (Ugani) wawili na wanavijiji/viongozi wanne.

b) **Ushiriki katika Kitongoji/Mtaa**

- Timu za ushiriki kwa msaada wa Mwenyekiti wa kitongoji, ziandae na kuwezesha mikutano ya makundi ya watu mbalimbali katika kitongoji.
- Katika mikutano hii watu hujadili hali halisi, matatizo na vikwazo vya maendeleo, fursa zilizopo kutatua matatizo yao, kupanga safu za matatizo na fursa ili kutoa vipaumbele, kuweka malengo na dira ya shughuli za kufikia malengo, bajeti/nyenzo na jinsi rasilimali hizo zinavyopatikana, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini.
- Uchambuzi wa matatizo, fursa na vikwazo hujumuisha huduma za jamii kama vile elimu, afya, maji, nishati, miundombinu, na msingi wa uchumi katika jamii kama vile matumizi ya ardhi, maliasili, kilimo, mifugo, uvuvi, madini n.k.

- Kama sehemu ya mpango, jamii hujadili na kupanga matumizi ya ardhi na usimamizi wake.
- Jamii katika kitongoji huwezeshwa kuweka maafikiano katika miniti/mihtasari na jedwali la mfumo wa Mpango wa Kazi wa Jamii.

c) Ushiriki katika Kijiji/Mtaa

- Halmashauri ya Kijiji/Kamati ya Mtaa hukutana na Timu ya Wawezeshaji kupokea na kujadili mipango ya vitongoji au sehemu za mtaa.
- Halmashauri ya Kijiji/Kamati ya Mtaa huweka malengo na dira ya kijiji/mtaa, na hatimaye vipaumbele vya kijiji/mtaa kwa kuzingatia rasilimali zilizopo na misaada inayopatikana toka nje
- Halmashauri ya Kijiji/Kamati ya Mtaa hukutana na kujumuisha mipango ya taasisi nyingine za kidini, mashirika ya kujitolea na vikundi vya wananchi, miradi binafsi, pamoja na miradi inayofadhiliwa.
- Halmashauri ya Kijiji/Kamati ya Mtaa huhakikisha kila shughuli iliyopangwa inatengewa fedha katika Bajeti na vyanzo vya fedha na rasilimali nyinginezo vinajulikana.
- Shughuli zitakazofanywa kwa nguvu ya wananchi huelezwa wazi katika mpango shirikishi.
- Halmashauri hujadili matatizo yaliyopo katika matumizi ya ardhi na fursa za utatuzi wake, ili kuwa na mpango wa matumizi ya ardhi ya kijiji na usimamizi wake.

Halmashauri huweka maafikiano katika miniti/muhtasari na jedwali la mfumo wa mpango wa kazi wa jamii.

Jedwali linakuwa katika mfumo ufuatao:

Malengo	Shughuli	Rasilimali/ Bajeti	Muda	Watendaji	Matokeo	Ufuatiliaji/ Tathmini

Halmashauri ya Kijiji/Kamati ya Mtaa huandaa Mkutano Mkuu wa kijiji/Mtaa ili kujadili kwa kina na hatimaye kupitisha mpango Shirikishi wa Maendeleo ya Kijiji/Mtaa.

3. Mwisho

- Ni muhimu kwa viongozi kuhakikisha kuwa mikutano katika ngazi mbalimbali inaitishwa na kuhudhuriwa na watu inavyopaswa, kwa kuzingatia koramu, ili maamuzi yawe ya wengi katika misingi ya demokrasia.
- Makundi mbalimbali ya watu, kijinsia, kiumri, kiuchumi-jamii, kidini, yahamasishwe kuhudhuria mikutano hii na kupewa fursa ya kutoa maoni na utashi wao.